

# JE, WATOTO WETU WANAJIFUNZA?

## Ripoti ya Tathmini ya Kujifunza ya Uwezo Tanzania, 2019

**UTANGULIZI**

**ZAIDA MGALLA, MENEJA WA UWEZO TANZANIA**

Uwezo ni moja ya programu muhimu za Twaweza (www.twaweza.org ). Inafanya tathmini kubwa zaidi Afrika inayoendeshwa na wananchi juu ya matokeo ya kujifunza ya watoto katika nchi tatu za Afrika Mashariki: Kenya, Tanzania na Uganda. Lengo la tathmini ya kujifunza ya Uwezo ni kufuatilia na kubainisha hali halisi ya matokeo ya kujifunza hasa stadi muhimu za kusoma, na kufanya hesabu kwa watoto wenye umri wa miaka 6-16. Tanzania ni miongoni mwa nchi za Afrika zilizodhamiria kutoa elimu bora kwa wote kama ilivyoainishwa kwenye malengo

127 Barabara ya Mufinga, ikipakana na Barabara ya Kinondoni.
S.L.P 38342, Dar es Salaam, Tanzania.

Simu: +255 22 2664301-3
bp: info@twaweza.org | www.uwezo.net

ya kidunia ya Elimu kwa Wote (EFA 1990, UNESCO 2000, UNESCO 2009) huku mkazo ukielekezwa zaidi kwenye kuinua ubora wa elimu na kukuza stadi za msingi za kusoma, na kufanya hesabu, ambazo pia zipo kwenye Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Elimu (Sustainable Development Goals, SDG4). Utafiti wa Uwezo unatuwezesha sisi sote kujua endapo uwekezaji (fedha, nguvukazi) ambao umefanywa kwenye utoaji wa huduma bora za elimu kwa watoto unaleta matokeo yaliyotarajiwa. Uwezo inafanya hilo kwa kutoa ushahidi madhubuti wa juu ya viwango vya ujuzi wa kusoma na kufanya hesabu kwa watoto wenye umri wa kwenda shule. Tathmini za Uwezo hutoa takwimu muhimu zinazoibua mijadala ya umma juu ya sera ya elimu na mafanikio ya utekelezaji wake

Ushirikishwaji wa wananchi wa kujitolea ni nguzo ya tathmini za kujifunza za Uwezo. Wananchi hawatazamwi kama watumiaji tu wa taarifa za tathmini ya Uwezo, bali pia wanatumika kama wadau wakuu katika upatikanaji wa takwimu na vyanzo vya maarifa. Uwezo inayashirikisha mashirika rafiki ya ndani ya wilaya katika kuratibu shughuli za tathmini kwenye kila wilaya zilizochaguliwa kwenye mikoa yote ya Tanzania Bara. Kwa upande wake, mashirika rafiki huajiri wahojaji wa kujitolea wapatao 60 wanaotoka vijiji 30 ili kusaidia kukusanya takwimu katitak kaya zilizochaguliwa kwenye kila wilaya. Kaya ishirini katika kila kijiji hutembelewa na, kwa ridhaa ya wazazi, watoto wote wenye umri wa miaka 6 hadi 16 katika kaya hizo hufanyiwa tathmini. Takwimu za viashiria vya ngazi ya shule pia hukusanywa kutoka kwenye shule moja ya msingi ambayo watoto wengi wa kila eneo lililofanyiwa tathmini wanasoma hapo. Kwa njia hii, Uwezo huzalisha takwimu muhimu ndani ya nchi kupitia watu na mashirika yaliyopo kwenye jamii husika, jambo ambalo linahimiza ushiriki wa ndani na umiliki wa matokeo.

Mwaka 2017, Uwezo Tanzania ilifanya tathmini ya sita ya ujifunzaji katika wilaya 56 za Tanzania Bara. Tathmini hiyo ilifanywa kwenye Maeneo ya kuhesabia 1,677 yaliyoidhinishwa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), na kuzifikia kaya zipatazo 25,532. Pia karibu watoto 64,639 wenye umri wa miaka 3-16 walishiriki kwenye tathmini. Kati ya hao, takribani watoto 48,530 wenye umri wa miaka 6 hadi 16 walipimwa uwezo wao wa kusoma, na kufanya hesabu rahisi za kiwango cha darasa la pili. Lengo la msingi la tathmini ya Uwezo linaendelea kubaki kuwa ni kukusanya takwimu huru juu ya viwango halisi vya ujuzi wa kusoma, na kufanya hesabu kwa watoto wenye umri wa kwenda shule. Kwa kuzingatia kasi kubwa iliyopo ya maboresho ya sera, hitaji la uwepo wa takwimu madhubuti ili kutathmini matokeo ya programu mbalimbali za elimu, sera na bajeti juu ya matokeo ya ujifunzaji ni jambo la muhimu sana, hasa kwa kuzingatia mwelekeo mpya wa kitaifa na kimataifa wa kutoa elimu bora kwa watoto wote.. Tathmini hii pia inachunguza viashiria vingi kuhusu mazingira ya kujifunzia na mambo muhimu ambayo yanaweza kuathiri matokeo ya kujifunza, kama vile hali ya kiuchumi na kijamii ya kaya, kiwango cha elimu ya wazazi, ushiriki wa wazazi kwenye mchakato wa elimu ya watoto wao, na kiwango cha ukaguzi wa shule kwa ajili ya kuthibiti ubora.

Matokeo ya mwaka huu yanahitaji kutafsiriwa kwa muktadha wa mabadiliko yanayotokana na utekelezaji wa Sera mpya ya Elimu na Mafunzo ya Tanzania ya mwaka 2014. Sera mpya inasema kuwa watoto wote walioandikishwa kuanzia darasa la kwanza shule ya msingi tangu mwaka 2016 na kuendelea watapata miaka kumi ya ElimuMsingi bure na ya lazima kwa wote: miaka sita ya elimu ya msingi na miaka minne ya elimu ya sekondari. Sera hii pia inaendelea kusisitiza watoto wapati elimu ya awali ya lazima angalau mwaka mmoja, pia sera imepunguza umri wa kuandikishwa kuanza elimu ya msingi kutoka miaka saba hadi sita. Sera ya Elimu pia imeweka mkazo zaidi wa kufundisha stadi za msingi za KKK (Kusoma, Kuandika na

Kuhesabu) kwa darasa la 1-2 na kuanza kufundisha somo la Kiingereza kwa watoto wakifikapo darasa la 3. (Ripoti ya Human Rights Watch, 2017)

Ripoti hii ni muhutasari wa matokeo ya tathmini ya mwaka 2017. Ripoti inaanza kwa kuainisha ukweli muhimu unaotokana na matokeo ya tathmini ili kuwawezesha wasomaji kupata dondoo muhimu za matokeo ya tathmini yaliyoanishwa katika ripoti hii. Ripoti hii imegawanyika katika sehemu kuu nne. Sehemu ya 1 ni utangulizi unaoelezea tathmini ya Uwezo na malengo yake. Sehemu ya 2 inatoa muhtasari wa mbinu iliyotumika kuchagua sampuli, kuandaa majaribio, mchakato wa kupata mashirika wadau na kuwapatia mafunzo kuhusu mchakato na zana za ukusanyaji wa takwimu na ukaguzi wa awali wa madodoso. Sehemu ya 3 inawasilisha matokeo muhimu ya tathmini ya mwaka huu na inachambua mwenendo na mabadiliko ya matokeo ya ujifunzaji tangu mwaka 2011 juu ya viwango vya kusoma, na kufanya hesabu kwa watoto walioko shuleni na watoto walioko nje ya shule. Sehemu hii inachunguza pia uandikishwaji wa watoto, pengo la usawa wa kijinsia katika ujifunzaji , makazi na hali ya kijamii na kiuchumi ya kaya, na mambo ambayo yanaweza kuathiri matokeo ya kujifunza kwa watoto, kama vile; upatikanaji wa walimu na sifa zao, uwepo wa miundombinu ya shule na huduma, ukaguzi wa shule kwa ajili ya uthibiti wa ubora na ushiriki wa wazazi kwenye mchakato wa elimu ya watoto wao. Sehemu ya 4 inahitimisha ripoti na inatoa maoni juu ya sera na mambo ambayo yanaweza kufanyika ili kufanikisha utoaji wa elimu bora kwa wote. Pia kuna mfano wa Majaribio, orodha ya mashirika wadau, watunga majaribio, waratibu wa mikoa na wakufunzi ambao walishiriki na kusaidia utekelezaji wa tathmini ya kujifunza ya Uwezo mwaka 2017. Pia orodha ya wilaya na nafasi ya kila wilaya kwa matokeo imewekwa mwishoni kwenye viambatisho.

Ni matarajio yetu kuwa matokeo kwenye ripoti hii yanatoa maoni muhimu juu ya hali ya matokeo ya kujifunza nchini Tanzania - kwa viongozi wa sekta ya elimu, wadau wa elimu na umma kwa jumla. Takwimu hizi zinatoa changamoto kwa wadau wote kutafakari juu ya hatua zinazoweza kuchukuliwa na mtu mmoja mmoja au kwa pamoja ili kuboresha elimu ya watoto wetu. Ripoti hii pia inabainisha hitaji la serikali kushughulikia pengo la usawa kwenye matokeo ya kujifunza, kwa kubaini maeneo ambayo yanahitaji uharaka wa kupewa kipaumbele katika mgawanyo wa rasilimali ili kuhakikisha kila mtoto wa Kitanzania anapata fursa sawa ya kwenda shule na kujifunza kikamilifu.

## Mambo Muhimu kutoka Tathmini ya Uwezo ya Mwaka 2017

Sehemu hii inaonesha Mambo muhimu 10 kutoka Tathmini ya Kujifunza ya Uwezo iliyofanyika mwaka 2017 ambayo iliangalia matokeo ya kujifunza ya watoto wenye miaka 6-16, na fursa ya watoto kwenda shule na mambo muhimu yanayohusiana na mazingira yao ya kujifunzia.

### Matokeo ya Kujifunza

Mambo muhimu juu ya matokeo ya kujifunza yametokana na viwango vya ufaulu wa majaribio ya kusoma na kufanya hesabu yaliyotolewa na Uwezo Tanzania, katika kusoma (Kiswahili, Kiingereza) na kufanya Hesabu hadi ngazi ya kutoa). Watoto waliopewa majaribio haya walikuwa makundi yafuatayo: (a) watoto wote wenye umri wa miaka 9-13 (waliopo shuleni na nje ya shule) (b) watoto (wanaosoma shule) walio darasa la 3 na darasa la 7, (c) watoto ambao hawasomi shule kabisa wenye umri wa miaka 9-13. Watoto wote walipimwa uwezo wao kwa majaribio ya ngazi ya darasa la 2 kwa masomo yote matatu.



# MAMBO KUMI MUHIMU KUHUSU MATOKEO YA KUJIFUNZA



## JAMBO LA 1

**Ujuzi wa kusoma Kiswahili umeongezeka.**

Asilimia ya watoto wa darasa la 3 ambao waliweza kusoma hadithi fupi ya Kiswahili imeongezeka mara mbili zaidi kati ya mwaka 2011 na 2017.





Ujuzi wa kusoma kwa wanafunzi wa darasa la 7 haujaongezeka sana. Takwimu za mwaka 2017 zinaonesha kuwa, wanafunzi 14% wa darasa la 7 wanamaliza shule ya msingi hawawezi kusoma hadithi ya darasa la 2.



## JAMBO LA 2

**Ujuzi wa kusoma Kiingereza uko chini na unaendelea kushuka.**





Matokeo ya tathmini za miaka mitatu iliyopita yanaonesha kushuka kwa viwango vya ufaulu somo la Kiingereza kwa wanafunzi wa darasa la 7.



## JAMBO LA 3

**Viwango vya ujuzi wa kuhesabu vimebadilika kipindi hadi kipindi na vinaonesha kuboreka kidogo.**

Katika ripoti hii kiwango cha juu cha ujuzi wa kufanya hesabu kiliwekwa kuishia tendo la kutoa kulingana na mtaala wa kitaifa wa sasa wa hesabu za darasa la 2. Viwango vya ufaulu wa majaribio ya hesabu kwa wanafunzi wa darasa la 7 vimeshuka kutoka 88% mwaka 2014 hadi 80% mwaka 2017. Matokeo ya kutia moyo zaidi yalionekana kwa watoto wa darasa la 3 ambapo ufaulu wao uliongezeka.







## JAMBO LA 4

**Kwa ujumla, kiwango cha ujuzi wa kusoma na kuhesabu kwa watoto kimeboreka kiasi kati ya mwaka 2011 na 2017**



Watoto wenye umri wa miaka 9-13 (ikijumuisha wasiokwenda shule) walifaulu majaribio ya Uwezo yaliyopima ujuzi wa kusoma na kuhesabu.



## JAMBO LA 5

Tofauti kubwa kwenye matokeo ya kujifunza ilibainika kati ya wilaya moja hadi nyingine

Kwa wastani,

WATOTO **7** KATI YA 10

wenye umri wa miaka 9-13 walifaulu majaribio ya kusoma na kufanya hesabu kwenye wilaya kumi zenye ufaulu wa juu ikilinganishwa

WATOTO **3** KATI YA 10

na watoto 3 tu kati ya 10 waliofaulu majaribio hayo kwenye wilaya kumi zenye ufaulu duni. Wastani wa ufaulu ulianzia

73%

WILAYA YA MERU

NA WA CHINI


24%

WILAYA YA NZEGA

**Hali ya uandikishwaji shuleni**

## JAMBO LA 6

Watoto wengi zaidi wa umri wa miaka 6 kwa sasa wameandikishwa shule ya awali au shule ya msingi



35% **Mwaka 2015 (wote wakiwa shule za awali)**

78% **Mwaka 2017 (41% wakiwa kwenye shule za awali na 37% shule za msingi)**

## JAMBO LA 7

Watoto wengi wa shule za msingi wanaacha shule wakiwa madarasa ya mwanzoni kuliko madarasa ya juu

70%

ya watoto ambao waliacha shule walifanya hivyo wakiwa madarasa ya mwanzo shule ya msingi.

Kwa mfano, wastani wa watoto walioacha shule wakiwa darasa la kwanza, ni 23,5%, la pili 20% na la tatu ni 27.5% .

Kwa darasa la 7 walioacha shule walikuwa 4.5%



**Mazingira ya Kujifunzia**

## JAMBO LA 8

**Viwango vya ukaguzi wa shule kwa ajili ya kuthibiti ubora vinatofautiana sana wilaya moja na nyingine**

Kwa wastani,

77%

SHULE **3** KATI YA 4

zilizofanyiwa utafiti zilikuwa zimekaguliwa kwa ajili ya uthibiti ubora mwaka 2017. Hata hivyo, viwango vya ukaguzi vilitofautiana sana.

Wilaya ya Iringa Mjini

**100%**

Wilaya ya Uyui

**43%**

## JAMBO LA 9

**Nusu ya wazazi wote waliwatembelea walimu wa watoto wao mwaka 2017.**



50% wanawatembelea walimu wa watoto wao. kuna tofauti kubwa ya ushiriki wa wazazi ki-wilaya.

wazazi 9 kati ya 10 Wilayani Iringa Mjini

wazazi 3 kati ya 10 (32%) Wilayani Nzega

## JAMBO LA 10

**Shule 1 kati ya 4 za Tanzania bara zinatoa chakula kwa wanafunzi**

23%


Shule 1 kati ya 4 zinatoa chakula kwa wanafunzi

Tofauti ni kubwa sana kati ya wilaya na wilaya kwenye utoaji wa chakula kwa watoto shuleni



**0%**

Wilaya za Rorya, Buhigwe, na Ukerewe




Wilaya ya Moshi